**SHULE YA SEKONDARI KANOMBE/EFOTEC**

**KIDATO CHA KWANZA**

**MAZOEZI YA KUFANYIA NYUMBANI**

**Soma wimbo huu kasha ujibu maswali yanayofuata**

Mimi ni **stuli**, watu hunikalia
Mimi ni **mwiko**, mama hunipikia
Mimi ni **mto**, mimi hunilalia
Mimi ni **mlango** ,nafunga ili kulinga wanoingia
Mimi ni **dirisha**, hewa safi kuingia
Mimi ni **kijiko**, kupakua chakula
Mimi ni **sebule**, wageni kukaribisha
Mimi ni **chumba cha malazi**, mwenye nyumba njoo
Mimi ni **veranda** , keti hapo nje
Mimi ni **kochi**, kukalia ama kuketia
Mimi ni **karai**, ukitaka kuoga

Mimi ni **paa**, nakaa juu ya nyumba

Mimi ni **sahani** , chakula kulia hapo

**Kikombe** cha kunywa maji, **kitanda** kulalia

**Kabati** kuweka vitu, na **uma** kumegea chakula

**Runinga** kupata habari na **redio** dada yake

**Zulia** kupamba nyumba na **vitambaa** kuirekebisha

Kusema kweli wenzangu, nyumba ina mengi.

**MASWALI YA UFAHAMU**

**CHAGUA JIBU SAHIHI ILI KUJAZA SENTENSI/**

1 . Kazi ya dirisha ni…………………...... hewa ndani ya nyumba(kuleta / kutoa)
2. kifaa kinachotumiwa kulala juu yake ni ………………...( chumba cha malazi/ kitanda)
3. Veranda inapatikana ……………………… ya nyumba (sebuleni, nje ya nyumba)
4. ……………………………….. hutumiwa jikoni( mwiko/ kochi)
5. Zulia hupatikana…………………………………(sebuleni/ nje ya nyumba)

**Kamilisha maamkizi ya hapo chini baina ya mama na Kayitesi/**

Kayitesi : hodi !

Mama : …………………………………………..

Kayitesi : shikamoo mama!

Mama : ……………………………! Hujambo ?

Kayitesi :……………………………………

Mama : habari za masomo ?

Kayitesi : ……………………………………………

Mama : haya karibu mezani upate chakula.

Kayitesi :……………………………………………

**Jaza jedwali ifuatayo kwa kutumia maamkizi**

| **Maamkizi** | **Jibu** |
|---|---|
| **Hamjambo ?** | **…………………………………………………** |
| **.......................................................** | **Ya kuonana !** |
| **Sabalheri !** | **………………………………………………** |
| **………………………………** | **Nishapoa !** |
| **Usiku mwema !** | **………………………………………………** |
| Hujambo | ……………………………………………….. |
| ………………………………………. | Marahaba |
| Pole dadangu | ………………………………………………… |
| ……………………………………….. | Binuru |

**Chagua jibu sahihi kutoka kwa majibu yaliyo mabanoni a kujaza sentensi**

**Mf :** …………………………..ninaitwa Nshuti ( wewe, mimi)

**Jibu : mimi** ninaitwa Nshuti

1. Wewe ……………………….. ( unanikumbuka, ninakukumbuka)
2. ……………………………….. anaitwa Samantha. ( yeye , wewe)
3. ………………………………..mnaitwa ( nyinyi, wao)
4. ……………………………….wanasoma( wewe, wao)
5. ……………………………….tunalima. ( mimi, sisi)

**Tulisoma uundaji wa silabi katika Kiswahili. Toa mifano miwili (2) ya maneno yenye silabi zinazoundwa na:/ 3**

a) Irabu pekee: 1. ………………………… 2 ……………………………
b) Konsonanti pekee: 1. ……………………. 2.…………………………..…
c) Konsonanti + irabu: 1 …………………… 2.…………………………..…

**Husisha vifaa vya shuleni katika sehemu A na kazi ya vifaa hivyo katika sehemu B /3**

| SEHEMU **A** | SEHEMU **B** |
|---|---|
| 1. Kifutio | A. Kuchora picha |

| | |
|---|---|
| 2. Chaki | B. Kupiga mstari |
| 3. Kitabu | C. Kuandika masomo na mazoezi |
| 4. Kabati | D. Kujulisha wakati |
| 5. Penseli | E. Kuweka vitabu |
| 6. Rula | F. Kukaa, kuandika na kuweka vitabu vya wanafunzi |
| 7. Daftari | G. Kukaa |
| 8. Saa | H. Kuandika ubaoni |
| 9. Kiti | I. Kufuta ubao |
| 10. Dawati | J. Kusoma |

Jaza sentensi zifuatazo kwa kuchagua neno moja kati ya maneno haya **: muhula, Kiranja, mtihani, Mkuu, sare, wanatushauri, wavulana, mabwenini, bwaloni, mchana, anachunguza.**

**Mfano**: walimu washauri ……………………………kuheshimiana na wenzetu

**Jibu**: walimu washauri **wanatushauri** kuheshimiana na wenzetu.

1. Huu ni ………………………………..wa kwanza wa mwaka wa shule
2. Tunafanya …………………………wa Kiswahili. Mwalimu wetu ametupatia maswali rahisi.
3. Wanafunzi wote wa shule yetu wanavaa……………………………………
4. ……………………………………wa darasa letu anaitwa Kagabo. Yeye anasimamia wanafunzi wenzake.
5. …………………………………wa shule yetu ni mzuri sana. Yeye anaongoza shule vizuri.
6. Mwalimu mshauri wa wasuchana ……………………………………nidhamu ya wasichana
7. Mwalimu mshauri wa ……………………………….anapanga michezo shuleni
8. Wanafunzi wanalala …………………………………………………
9. Walimu washauri wanaingia ………………………kuchunguza chakula chetu.
10. Wakati wa chakula cha ……………………….tunaenda bwaloni.

**Tummia mshale kuhusisha majina katika A na maelezo katika B**

| **SEHEMU A** | **SEHEMU B** |
|---|---|
| 1. Mkuu wa shule | **a)**Kufundisha wanafunzi |
| 2. Mhasibu | **b)**Kuchunguza nidhamu ya wasichana na kuwashauri |
| 3. Kiranja | **c)**Kutunza vitabu makitabani |
| 4. Mwalimu wa nidhamu | **d)**Kusoma |
| 5. Mwalimu wa mitaala | **e)**Kuchunguza nidhamu ya wavulana na kuwashauri |
| 6. Mwalimu mshauri wa wasichana | **f)**Kusimamia wanafunzi wenzake |
| 7. Mwalimu mshauri wa wavulana | **g)**Kuchunguza nidhamu ya wanafunzi |
| 8. Walimu | **h)**Kupokea karo za shule |
| 9. Wanafunzi | **i)**Kupanga masomo ya wanafunzi |
| 10. Mkutubi | **j)**Kuongoza shule |

**Jeuza sentensi zifuatazo katika umoja au wingi**

**1.** Mimi ninasoma vizuri……………………………………………………………..
**2.** Wao hawasomi Kiswahili……………………………………………………………
3. Mtoto huyu anafua nguo……………………………………………………………..
4. Kalisa anasaidia mtoto yatima………………………………………………………….
5. Nyinyi mnavua samaki kila siku………………………………………………………

**Eleza misamiati ifuatayo**

a) Nadodha : ………………...……………………………………………………….
b) Hakimu : ……………………………………………………………………….
c) Rubani : ……………..…………………………………………………………..
d) Mfinyanzi : ………………………………………………………………......
e) Dobi ……………………………………………………………………………….

**Jaza jedwali ya hapo chini. Tumia V ili kuhusisha aina ya kazi ya mwanafunzi na mahali kazi hiyo inapotokea**

| AINA YA KAZI | KAZI YA NYUMBANI | KAZI YA DARASANI |
|---|---|---|
| **Kupiga mswaki** | | |
| **Kuchota maji** | | |
| **Kufuta ubao** | | |
| **kulima shamba** | | |
| **Kufanya jaribio** | | |
| **Kupika chakula** | | |
| **Kuvaa sare** | | |

***GOOD LUCK !!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!!***